MWONGOZO WA KIGOGO

JALADA LA KIGOGO.

Michoro kwenye jalada

1. Mchoro wa ramani ya Afrika uliochorwa kwa rangi nyeusi. Mchoro huu ni ishara wazi kuwa manthari husika ni Afrika.
2. Mchoro wa watu waonekanao kama vivuli kwenye mchoro wa ramani ya Afrika. Pia ni rangi nyeusi kiashiria watu wa bara la Afrika.
3. Mchoro wa jua lichomozalo hasa nyuma ya ule mchoro wa ramani ya bara la Afrika. Mwanga wa jua lenyewe ni rangi ya manjano ishara ya tumaini licha ya matatizo yawakumbao waafrika. wanamapinduzi wanapigania haki ili kujenga jamii mpya.
4. Mchoro wa mtu chini kushoto mwa jalada la mbele. Amevalia kofia, ana fimbo mkononi na amekalia kiti cha kifahari...pia amechorwa kwa rangi nyeusi. Anaashiria kiongozi(kigogo) wa kisiasa tena mwafrika.
5. Mchoro wa maji hasa huenda ni bahari kati ya mchoro wa ramani ya bara la Afrika na yule mtu mwenye kuketi kwenye kiti cha kifahari. Ni kweli kwani bara la Afrika limezungukwa na bahari.

Maana ya rangi kwenye jalada

1. Nyeusi imetanda sana na hata kukolezwa zaidi ya rangi nyinginezo. Inatumika kuashiria yafuatayo...
    - ✓ Jumuia ya Afrika.
    - ✓ Mauti au kifo.
    - ✓ Matatizo aina aina.
    - ✓ Kiza au majira ya usiku.
2. Manjano imetumika kwenye mchoro wa jua na maandishi mbele na nyuma mwa jalada. Rangi hii inaashiria mwangaza na tumaini
3. Kijivu pia imetumika japo kwa mbali sana. Ina maana ya mwanga wa kiasi, wema wa shaka au matatizo
4. Udhurungi inaonekana kwa mbali pia. Inaashiria utajiri au ufalme
5. Nyeupe ipo japo lazima uwe mwangalifu na inaashiria wema na bahati
6. Hivyo basi, jalada hili ni kama muhtasari wa Tamthilia nzima jinsi tutakavyoona kwenye uchanganuzi wake wa kine mbeleni.

UFAAFU WA ANWANI KIGOGO

Kigogo ni mtu mwenye mamlaka kubwa, Kulingana na tamthilia hii, kigogo ni mtu mwenye madaraka makubwa ya kiutawala. Anafahamika na wengi hasa vibaraka wake kama kigogo

(1) Majoka Anatumia Mamlaka Yake Kuwanyanyasa Wananchi Wa Sagamoyo Kwa Kuwatukana,

(2) Majoka anatumia mamlaka yake kutangangaza Kipindi Cha Mwezi Nzima Cha Kusherekea Uhuru

(3) Majoka anatumia mamlaka yake Kufunga Kwa Soko La Chapakazi Ili Aweze Kujenga Hoteli Ya Kifahari,

(4) Majoka anatumia mamlaka yake kupandisha Bei Ya Chakula kiwandani

(5) Majoka anatumia Mamlaka Yake Kumtendea Ashua Ukatili Kwa Kuwa Majoka Alikuwa Anatamani Ashua kimapenzi

(6) Kutokana Na Mamlaka Wa Majoka Anaamuru Wanapolisi Kutawanya Waandamanaji wanaopinga uongozi wake

(7) Majoka anatumia mamlaka yake kumpa Mamapima Kibali Cha Kuuza Pombe Haramu Kwa Wananchi Wa Sagamoyo

(8) Majoka anatumia Mamlaka Yake Kufunga Vyombo Vya Habari(runinga) ili yake pekee ibaki
(9) Majoka anatumia mamlaka yake kupanga Kifo Cha Jabali Mpinzani wa kisiasa
(10) Majoka anatumia mamlaka yake kuamuru wauni wke wamwangamize Tunu Mpinzani. Tunu anabahatika kwani analemazwa tu
(11) Majoka anatumia mamlaka yake pia kuzima uchunguzi wa Tunu kuhusu kifo cha Jabali

PLOTI…… …… **(KWA NAKALA NZIMA PIGA SIMU 0724351706)**

MAUDHUI.

MIGOGORO

. (i) **Mgogoro kati wa wanandoa Ashua na Sudi.**
Mgogoro huu ulichochewa na hali ngumu ya maisha ambapo Ashua anapotiwa kizuizini anasema amechoka kumuona Sudi akifuatana na Tunu. Pia anamlaumu mumewe kwa kushindwa kuikimu familia yake.
Suluhisho: Sudi anamshawishi mkewe asisikize umbea wa watu kama Majoka.

(ii) Mgogoro kati ya Viongozi na wanaharakati.
Unachochewa na uongozi mbaya wa Majoka. Majoka anafunga soko la chapakazi na Tunu anaongoza watu kuandamana ili lifunguliwe.
Suluhisho: Wanasagamoyo wanamwondoa Majoka mamlakani.

(iii) Mgogoro baina ya mafundi wa kuchonga vinyago.
Sudi na Boza wanagombana kwa sababu ya mitazamo yao. Boza ametosheka na uongozi wa Majoka ilihali Sudi anaupinga.
Suluhisho: Sudi anawasihi waungane naye na hatimaye kombe anazinduka.

(iv) Mgogoro wa nafsi (majoka)
Babu anaichochea nafasi ya Majoka kuwa abadilishe mawazo na mienendo yake kwani wema hauozi.
Suluhisho: Majoka anakataa kuzinduka na hivyo haukusuluhishwa.

(v) Mgogoro baina ya vyombo vya habari na utawala.
Hii ni kutokana na hatua mbalimbali zinazohusu udhalimu wa serikali. Runinga ya mzalendo inapigwa marufuku baada ya kupeperusha habari kuhusu umaarufu wa Tunu.
Suluhisho: Watu wanauangusha utawala mbaya wa Majoka.

(vi) Mgogoro baina ya Majoka na Sudi.
Unatokana na kuwa wote wawili walimpenda Ashua. Majoka anataka Ashua amwache Sudi ili amwoe.
Suluhisho: Sudi anamhakikisha Ashua kuwa annemtunza na kumwomba asititilie maanani umbeya wa Majoka.

(vii) Mgogoro baina ya nguruno na Sudi.
Ngurumo anamtuhumu Sudi kwa kusema kuwa alilala na Tunu
Suluhisho: Sudi hakumhjali bali aliendelea na harakati na Tunu aliendelea na za kuwazindua wanajamii.

(viii) Mgogoro kati ya Kenga na Majoka.
Kenga anakengeuka na kukubaliana na waandamanaji.
Suluhisho: Kenga anaungana na waandamaji na hatimaye kuangusha utawala wa Majoka.

(ix) Mgogoro kati ya Majoka na Kingi.

Kingi anakataa kutii agizo la kuwapiga risasi wananchi waliokusanyika katika soko la Chapakazi.
Suluhisho: Wanaouangusha utawala mbaya wa Majoka.

(ix) Mgogoro baina ya Tunu na Ngurumo.
Ngurumo anamdunisha Tunu huku akisema kuwa hawezi kupatia/kupiga kura yake kwake. Hata anamwimbia wimbo.
Suluhisho : Tunu na Sudi wanamwacha ngurumo mangweni.

(ix) **Mgogoro kati ya Husda na Ashua.**
Husda anamchukia na kumpiga Ashua kwa kumtaka mumewe.
Suluhisho: Ashua anatiwa korokoroni.

(xii) **Majoka na wananchi.**
Wananchi wanajitokeza kuandmana ili kupinga uongozi mbaya wa Majoka. Majoka anamwamuru Kingi awapige risasi lakini alikataa.
Suluhisho: Wananchi wanauangusha utawala wa Majoka.

UKIUKAJI WA HAKI NA UVUNJAJI WA SHERIA

1) Majoka kuruhusu ukataji miti.
2) majoka kupatiana kibali cha uuzaji wa pombe haramu.
3) Soko la Chapakazi kufungwa.
4) Waandamanaji kupigwa bila kuleta ghasia (ni haki yao).
5) Kuamuru mkuu wa polisi (Kingi) awapige watu risasi.
6) Ashua kufungiwa seli bila hatia.
7) Majoka kumfuta Kingi kazi/chopi kutishwa atamwaga unga.
8) Jabali kuuawa/Ngurumo
9) Tunu kuvamiwa/kuumizwa
10) Kutishiwa kuuawa km Chopi alipangiwa kuuawa.
11) Sudi kushinikizwa achonge kinyago.
12) babake Tunu kuuawa katika kiwanda cha Majoka.
13) Vijana watano kuuawa wakati wa maandamano.
14) Kuongeza bei ya vyakula maradufu
15) Kubomoa vioski katika soko la chapakazi.
16) Majoka kumtaka Ashua kimapenzi
17) Wanafunzi shuleni kuadhibiwa watumie dawa za kulevya.
18) Uwanja wa soko kunyakuliwa.
19) Kutozwa kodi Zaidi
20) Kutosafisha soko ilhali watu wanalipa kodi
21) Kufungwa kwa vituo vya habari
22) Ngurumo kuzikwa juu ya maiti wengine.

……
……..

KWA NAKALA NZIMA ILIYO NA PLOTI, MAUDHUI, WAHUSIKA NA UMUHIMU WAO NA TAMATHALI ZA USEMI PIGA SIMU KWA NAMBARI 0724351706(BWANA CHEPKWONY)